NA:	NAMBARI:	
HULE:	TAREHE:	
	SAHIHI:	

D2/2
ISWAHILI
UGHA
ARATASI YA PILI
ULAI / AGOSTI 2016
IUDA: SAA 2 1/2

## JARIBIO LA MTIHANI WA MWAKA - 2016

KIDATO CHA 3

CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI

KISWAHILI &

LUGHA

KARATASI TA PILI

MUDA: 2 1/2

IAAGIZO

Andika jina lako na nambari katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

Jibu maswali yote.

Majibu yote yaandikwe katika hafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

### KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

### 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita: wanawake makamu ya nyanyake na mamake mkuu.

Yeye hutarajia kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke ' a bwana, kumzalia watoto na daima dawamu kuwa 'mwendani wa jikoni' akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. Akanyagapo muma nava papo huutia wayo wake.

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, Historia, Jiografia, Hesabu, Sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya, akataka kuwa mwalimu akawa. Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi. Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa hateswi akafyata ulimi. Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali 'mahali pake' katika jamii alipotengewa na wanaume wenye wawazo ya kihafidhina yaliyopitwa na wakati,

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake iwapo ni mfanyi biashara imepiga hatua ya kutomrudisha ukatani.

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo, lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanamume wa 'kisasa', ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama mshiriki sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya aushi.

Masy	vali vali	
(a)	<u>waii</u> (ii) Msemo 'mwendaniwa jikoni' unadhihirisha hali gani ya mwanam	nke katika jamii?
	tottee	(alama 1)
	(ii) Thibitisha hali uliyotaja hapo juu kwa kutoa hoja <u>nne</u> .	(alama 2)
(b)	Mwandishi ana maana gani anaposema 'akanyagapo mume naye p	papo huutia wayo wake' (alama 1)

(d) Eleza hoja sita zinazoonyesha kuwa wanaume wana 'mawazo ya kihafidhina' dhidi ya mwanamke. (alama 3)  (e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliyyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani: (ii) Aushi: (iii) Aushi: (iii) Aushi: (alama 15)	(c)	Tofautisha mwanamke wa kiasili na wa kisasa ukizingatia maswala ya ndoa	na elimu.
(d) Eleza hoja sita zinazoonyesha kuwa wanaume wana 'mawazo ya kihafidhina' dhidi ya mwanamke. (alama 3)  (e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:			(alama 4)
(d) Eleza hoja sita zinazoonyesha kuwa wanaume wana 'mawazo ya kihafidhina' dhidi ya mwanamke. (alama 3)  (e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:			
(d) Eleza hoja sita zinazoonyesha kuwa wanaume wana 'mawazo ya kihafidhina' dhidi ya mwanamke. (alama 3)  (e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa (alama 2)  (i) Ukatani:			
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi.  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa (alama 2)		이 경기를 하고 있다면 하는 사람들이 가장 하는 것이 되었다. 아이들은 것은 사람들은 것은 사람들이 가지 않는데 하는데 없다.	
(d) Eleza hoja sita zinazoonyesha kuwa wanaume wana 'mawazo ya kihafidhina' dhidi ya mwanamke. (alama 3)  (e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:		하는 사람이 그리다가 하는 것을 하는데 하는 것이 하는데 하는데 뭐 하나 나를 하는데 없다.	
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi.  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa (alama 2)  (i) Ukatani:	(4)		dhina' dhidi ya
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi.  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa (alama 2)  (i) Ukatani:	(a)	10 전 시간 이 이 경기 전쟁으로 가게 되었다. 그렇게 하는 것이 하는 것이 없는 것이 없는 것이 없는 것이 없다.	
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa (alama 2)  (i) Ukatani:		이용하다 내 내용하다는 얼마면서 보이지 그렇게 하는 것이라면 모든 물을 때 때문에 하는 것이다.	
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa (alama 2)  (i) Ukatani:			
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:			
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliyyotumika katika makala taarifa (alama 2)  (i) Ukatani:			
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:			
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:			
(e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi.  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:			
na mwandishi. (alama 2)  (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:	(e)	Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika	
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:	(-)	하게 그렇지 하게 되어 되었다. 그리고 하는 것이 하고 있다면 하는 사람들은 사람들이 되었다. 그리고 하는 그는 그는 그리고 하는데 그리고 있다.	
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:		Tia stiwariaisii.	
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarifa.(alama 2)  (i) Ukatani:		-direction	
(i) Ukatani:			
	(f)	Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala taarif	a.(alama 2)
		(i) Ukatani:	
and the control of th			
		"ite"	
UFUPISHO: (ALAMA 15)	UFUP	PISHO: (ALAMA 15)	

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibo maswali yanayofuata.

Katika karne hii ya kesho, urafiki ni ngome kuu duniani ambayo huhifadhi maslahi ya kila rafiki. Rafiki mwema humpenda mwenzake si kwa sababu ni tajiri ama ana cheo kikuu nchini. mwadilifu huridhika na hali aliyonayo rafikiye; akiwa ni tajiri au ni maskini, ana cheo, hana. Rafiki mwema huwa mwadilitu wakati wowote. Wakati wa neema hushirikiana na rafikiye katika furaha na wakati wa shida hushirikiana naye katika huzuni na taabu zote zinazomkabili.

Sahibu mwema hutoa alichonacho kumkomboa rafiki yake, huwa radhi kabisa kufilisika kwa ajili vake. Mahali pa finyo hujasiri kuingia ili kumkomboa rafikiye, hushughulika zaidi kuliko wana ndugu wa toka nitoke. Kwa vyovyote hula naye tamu na chungu pamoja, mkono kwa mkono katika maisha yao yote hadi mmoja wao akaitoka dunia. Urafiki wa namna hii ndio ulefao Baraka ya Mungu, kuwashukia viumbe hao kama umande wa asubuhi.

Urafiki ni lazima sana katika maisha ya wanadamu. Urafiki ni mfano wa mishipa ipitishayo damu mwilini ili kurutubisha kila sehemu ya mwili. Ingawa ni bora kuwa na marafiki wengi lakini kila marafiki wanapozidi, ni hatari ya kuangukia kwenye marafiki wadanganyifu hasidi. Pasi na shaka, ni heri maadui kuliko marafiki wadanganyifu. Hivyo basi, tukiwa na rafiki walio kinyume cha wema na upole wa kulinda haki za wanadamu na wasiomcha Mungu ni lazima tuwaepuke. Ingawa na hivyo, vile vile sheria inatukataza tusisikilize au kujali ubaya wa mtu yeyote pasipo kuhakikisha. Huenda ikawa ni uvumi tu usiokuwa na msingi wowote. Ikiwa rafiki ni mbaya, haikosi atajulikana kwani mtungi mbovu haukawi kuvunjika. Lazima tuwapende watu wote ili kutimiza haki za kibinadamu na kuchukia matendo maovu. Rafiki waovu si vema kuwaacha katika maangamizi ya ubaya wao bali ni lazima tuwaambie waziwazi ili wapate kuokoka. Ukimsamehe rafiki, unaponya donda lake moyoni. Hivyo ni bora kuliko kumtaazama na hali anazidi kukosa.

### Maswali

(a)	Fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa kutumia maneno yasiyozidi 60. (alama	7, 1 ya mtiririko)
	<u>Matayarisho</u>	e mai sulla
	***************************************	
	······································	······································
	42	
	······································	
	· · · · · · · · · · · · · · · · · · ·	
		<b>V</b>
		***************************************
	<u>Jibu</u>	
	Jibu Kuruu Keek C	
	Jibu Jibu Karan Jiga Kan Jiga Karan Jiga Karan Jiga Karan Jiga Karan Jiga Karan Jiga Kar	
	Jibu III Jib	
	Jibu Heleko	
	Jibu Italian Heek Co	
	Jibu Resko	
	A Color of the Col	
	Jibu Kasa Qasa Qasa Qasa Qasa Qasa Qasa Qasa	
	A Color of the Col	
	A Committee of the comm	
	Add the state of t	
	A Complete C	

(b)	Fupisha	mambo mul	himu kama	yalivyoelezwa	na mw	andishi katika a	iya ya mwisho.	Tumia
	maneno	kati ya 60 - 6	65.		(	alama 8, 1 ya m	itiririko)	
	Matayar	isho						
		***************************************						
		,				- IT MEN		
							19	
						<sup>€</sup> O <sub>J</sub>		
						9120		
					1	call .	state unique	
						ano	M	Line to
		· ·			e Se	,. ,.		
74	Jibu				astpaper.	- Managara Takana	Selfred agreed Stim	OR THE
		)		ૂર્જ	303			
				SAC				
				W. H.				•••••
				iejt W				
			0	5				
		***************************************	* 6 <sub>06</sub>					
			-0 985 980	la de la companya de		e libera in the liberal		•••••
			HOS					
							***************************************	•••••
	•••••••						i	
							/	
	••••••	***************************************						
	••••••	••••••		• • • • • • • • • • • • • • • • • • • •		••••••		
		•••••••••••	•••••	•••••				
	••••••							

# ATUMIZI YA LUGHA i) (i) Tofautisha kati ya shadda na kiimbo . (aama 2) (ii) Tunga sentensi mbili kudhihirisha viimbo tofauti. (alama 2) (b) Eleza matumizi manne ya kikomo. (alama 4) (c) Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo: (alama 2) Amekwenda kucheza kandanda. (d) Tunga sentensi yenye muundo ufutao: (alama 1) W+T (e) Andika kwa ukubwa wingi: (alama 1) Mtu yule alicheza ngoma. (f) Yakinisha sentensi ifuatayo: (alama 1) Asiyesikia la mkuu huvunjia guu. (g) Bainisha sentensi ifuatayo. (alama 4) Rais Obama alizuru Kenya mwaka huu akapongezwa sana. (h) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi ya kivumisha cha - a - unganifu . (álama 2)

(i)	Tumia nomino ifuatayo kama kivumishi katika sentensi. Kijana.	(alama 1)
(j)	Andika kisawe cha rafiki.	(alama 1)
(K)	Kanusha : Huzuni alivaa nguo safi.	(alama 1
(i)	Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti sighuna.	(alama 2)
	- nATS	
(m)	Tunga sentensi <u>mbili</u> kuonyesha maana <u>mbili</u> ya maneno yafuatayo.  (i) ota  (ii) paa	(alama 2)
	(ii) paa	
(n)	Ainisha mofimu.	(alama 2)
	Andika katika kauli zilizopigwa mabanoni.  - La (Tendwa)  - Chota (Tendesha)	(alama 2)
	Toa maana <u>mbili</u> ya sentensi ifuatayo. Yakobo alimpigia Suleimani mpira.	(alama 2)
(q)	Huku ukitoa mifano, taja aina <u>mbili za</u> Nomino.	(alama 4)
V 41		

(r)	Mahali ambapo kulichafuka ni mwa Mwangi.	(alama 3)
(s)	Taja ngeli ya Nomino hii.	(alama 1)
(-/		
ISI	MU JAMII (ALAMA 10)	
(a)		(alama 4)
	. Child	
	120°	(
(b)	Fafanua sababu zozote tatu zinazopelekea mabadiliko ya sajili katika jamii.	(alama 6)
٠		******
	······································	
	- Visit	
	Ko X	
	49	
		***************************************